TANGAZO LA SERIKALI NA. 413 La Tarehe 24/05/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA 287)

---

# SHERIA NDOGO

---

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA, 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Same za Mwaka 2024.

Matumizi

2.Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuzoa taka.

"ada ya uchafuzi wa mazingira" maana yake ni malipo yanayotakiwa kulipwa kwa Halmashauri na kampuni, viwanda, kikundi, mtu binafsi na taasisi ambazo shughuli zao zinasababisha uchafuzi wa

mazingira; kwa kuzingatia kanuni ya mchafuzi kulipa (Polluter Pay Principle (PPP);

"adha" maana yake hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu na viumbe hai kwa ujumla;

"afya" maana yake hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala sio tu kutokuwa na ugonjwa au kilema;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa madawa;

"chanzo cha maji" maana yake ni eneo lolote ambalo limetunzwa kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii;

"choo bora" maana yake ni choo na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu;

"choo cha umma" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu kilichojengwa na

Halmashauri au wakala wake kwa matumizi ya umma;

"chukizo la afya" maana yake kitu chochote kinachoweza kuleta kinyaa machoni kwa kuona, kunusa, hewa chafu, madhara au kuhatarisha Afya za binadamu na wanyama;

"eneo la wazi" maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Same;

Sura ya 99

"hati ya usafi" maana yake ni hati inayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hii na Sheria ya Afya ya Umma na Kanuni zake;

"jengo la biashara" maana yake jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya biashara iliyokusudiwa;

"kaya" maana yake mtu mzima anayejitegemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye eneo la Halmashauri;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho

kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha-

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu;

(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa; au

(c) kuzaliana kwa wadudu hatari kama vile inzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"kituo cha taka" maana yake ni kizimba cha taka kilichowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye dampo la taka ngumu la Halmashauri;

"kupima afya" maana yake ni kupima afya katika vituo vya Afya vinavyomilikiwa na Halmashauri kubaini iwapo kuna vimelea vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi kisha kupewa cheti cha uthibitisho wa upimaji huo

Sura ya 191 "maji taka" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"mmiliki" maana yake ni mtu yeyote ambaye anamiliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za

starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote ndani ya eneo la Halmashauri;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mzalishaji wa taka ngumu" maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara au kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake za kila siku huzalisha taka ngumu;

"pipa la taka" maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira;

Sura ya 287 "Sheria" maana yake ni sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya;

Sura ya 191 "taka" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "taka ngumu" ina maana swa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"taka za majumbani" maana yake mabaki ya vyakula, maganda ya matunda, majivu, nguo chakavu, karatasi za aina mbalimbali, kinyesi cha mifugo, taka za bustani na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

Sura ya 191

"taka za viwandani" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira;

Sura ya 191

"uchafu hatari" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira;

"ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya nyumba, banda au zizi ndani ya eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii;

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

4.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi, mmiliki wa nyumba au mfanyabiashara kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake la biashara kwa kufanya yafuatayo:

(a) kukata au kupalilia majani yanayozunguka eneo la kuzunguka nyumba yake na mwanzo wa mipaka ya Barabara iliyopo mbele ya nyumba yake;

(b) kukusanya, kuhifadhi na kupeleka taka ngumu na laini ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara.

Usafi wa mifereji ya maji ya mvua

5.- Kila mmiliki wa nyumba atakuwa na wajibu wa kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mfereji wa maji ya mvua unaozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake au kiwanja chake na kuhakikisha mfereji huo unakuwa msafi na imara siku zote.

Siku ya kufanya ukaguzi wa usafi

6.- Kila siku ya Jumatano itakuwa ni siku maalum ya ukaguzi wa jumla wa usafi wa mazingira ambapo wakaguzi kutoka Halmashauri watapita kufanya ukaguzi wa mazingira na itakapobainika kuwa mtu yeyote hajafanya usafi au kuna uchafuzi wowote katika eneo husika, watachukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Usafi wa kila Jumamosi

7.- Kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa kila mwezi utafanyika usafi wa mazingira wa jumla kuanzia

saa 1:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi, ambapo kila mtu au taasisi itawajibika kushiriki katika zoezi la kufanya usafi wa mazingira na muda wote shughuli zote zitasimamishwa isipokuwa huduma muhimu kama zitakavyoainishwa na Halmashauri.

Kupaka rangi majengo

8.- Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha kwamba anapaka rangi nyumba yake au duka lake ndani na nje kila itakapochakaa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya mbu

9.- Itakuwa ni wajibu wa mmiliki wa nyumba au mpangaji kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo wa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

Biashara ya miwa na matunda

10.- Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ya matunda au miwa kuhakikisha kuwa ana chombo maalum cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Matengenezo ya magari, pikipiki, mitambo na kuegesha magari mabovu na uchomeleaji vyuma

11.- Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo na uchomeleaji vyuma vitatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa

baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri na kuwa na leseni ya biashara.

Marufuku

12.- (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote:

(a) kuendesha biashara ya upuliziaji dawa au biashara ya kuuwa wadudu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na awe na leseni iliyotolewa na Halmashauri;

(b) kusafisha shamba kwa kuchoma moto bila kibali kutoka kwa kamati ya mazingira ya Kijiji;

(c) kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote au kuchomelea vyuma katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo;

(d) kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo;

(e) kumiliki eneo la chanzo cha maji;

(f) kulima au kukata miti au kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 kutoka chanzo cha maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira;

(g) kufunga mtaa au barabara kwa shughuli

zozote bila kibali kutoka Halmashauri;

(h) kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai;

(i) kuuza bidhaa za chakula kwa kutandaza ama kupanga chini vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza;

(j) kuchinja au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;

(k) kutupa taka, uchafu wowote au kuacha taka mahali popote pasipotengwa kwa ajili ya shughuli hiyo;

(l) kutupa hovyo vitu kama vila vocha ya simu iliyokwisha kutumika, maganda ya muwa, majani ya mahindi, magunzi, chupa za vinywaji au kitu chochote kinachoweza kuchafua mazingira mahali ambapo siyo kwenye chombo cha takataka;

(m) kufungulia au kutiririsha au kuelekeza maji taka au kinyesi kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo au sehemu yoyote wakati wa mvua au wakati wowote kwenye mifereji ya maji ya mvua, mabonde au maji yanayotembea au sehemu nyingine yoyote isiyoruhusiwa;

(n) kuuza vyakula visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza;

(o) kupanga vyakula nje ya duka la vyakula; na

(p) mfanyabiashara, hospitali, taasisi, kaya, jengo au shughuli za viwanda kuchafua anga hewa kwa kuachilia moshi angani unaoweza kuleta madhara kwa binadamu, mimea na viumbe hai.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1)(b), kutakuwa na siku maalum itakayopangwa na Halmashauri ya Kijiji ya kusafisha shamba kwa kuchoma moto na watu wote waliopata kibali watasafisha mashamba yao siku hiyo.

(3) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hii kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(4) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hii ni kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa nne kamili asubuhi.

(5) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko.

Wajibu wa kulinda vyanzo vya Maji

13.- (1) Halmashauri itawajibika, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

(3) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri na jamii husika kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

Usafi wa mazingira

14.- Kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki jengo au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba:

(a) majani yanayozunguka jengo lake au makazi yanakatwa au kupaliliwa na kuondolewa katika eneo lake lote;

(b) taka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;

(c) maji taka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa maji taka;

(d) kuboresha na kupaka rangi jengo lake kila inapochakaa;

(e) kuwa na choo kilicho bora na kisafi wakati wote;

(f) atashiriki siku ya usafi ya Jumamosi ya kila

mwisho wa mwezi;

(g) ataondoa uchafu ikiwemo mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo katika mfereji wa maji ya mvua inayomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa safi wakati wote;

(h) kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuathiri upitishaji wa maji ya mvua na hivyo kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira kwa ujumla;

(i) anafanya uchambuzi wa taka;

(j) anahakikisha kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa katika eneo lilotengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka;

(k) anatunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vinavyowekwa na Halmashauri;

(l) kwa mfanyabiashara wa wa matunda au miwa kuhakikisha kuwa ana chombo maalumu cha kuhifadhia maganda au mabaki ya matunda.

Ada ya uzoaji taka

15.-(1) Kutakuwa na ada ya uzoaji taka katika kila kaya au mmiliki wa jengo ambayo itatozwa na Halmashauri kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoza ada ya utupaji wa taka katika eneo lililotengwa kutoka kwa mawakala, wamiliki wa taasisi mbalimbali, viwanda na makampuni pamoja na wazalishaji wengine wa taka kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(3) Ada ya uzoaji taka italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kieletroniki na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(4) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Wajibu wa kuwa na pipa la taka

16.- Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au mpangaji au mfanyabiashara kuhakikisha

kuwa ana chombo imara chenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa na Halmashauri au wakala kwa ajili ya kwenda kutupwa.

Kutupa taka Katika sehemu maalum

17.- Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba anatupa uchafu au taka katika vyombo maalum vilivyowekwa kwa ajili ya kutunzia taka katika maeneo maalum yaliyotengwa.

Uhifadhi majitaka

18.- Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

Taka za viwandani

19.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya na kusababisha kero kwa wakazi wa eneo la Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na taka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe wengine hai.

Kuweka eneo katika hali ya usafi

20.- Kila mwenye nyumba au eneo au mtu mwenye dhamana ya nyumba au eneo anatakiwa kuweka mazingira ya nyumba au eneo lake katika hali ya usafi

wakati wote na kuhakikisha hakuna taka zinazotupwa ovyo katika eneo lake.

Taka kutupwa kwenye gari la taka

21.- Kila kaya au wapangaji katika nyumba au wafanyabiashara watakuwa na jukumu la kutunza, kubeba na kupeleka taka walizozizalisha na kuzitupa moja kwa moja kwenye gari la kubeba taka kwa kuzingatia ratiba na utaratibu uliowekwa na Halmashauri au kuzitupa katika makasha ya taka yaliyowekwa katika baadhi ya maeneo.

Jukumu la kuwa na chombo cha kuhifadhia taka

22.- Kila mwenye nyumba au mpangaji, mmiliki au msimamizi wa eneo la biashara, taasisi na Ofisi ndani ya Halmashauri anatakiwa awe na pipa dogo au ndoo au chombo au kifaa chochote chenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia taka zinazozalishwa katika eneo hilo.

Wajibu wa mmiliki wa chombo cha usafiri

23.- Kila mmiliki au dereva wa chombo cha usafiri wa umma, kusafirisha mizigo, taka au madini ya ujenzi atawajibika-

(a) kuweka chombo au kifaa cha kihifadhia taka kwa ajili ya abiria wake;

(b) kuweka vifaa vya kufunika bidhaa anazosafirisha ili kutoruhusu bidhaa hizo kudondoka au kumwagika na kuchafua mazingira;

Machinjio na

24.- Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa duka

Maduka ya nyama

la kuuzia nyama kuhakikisha kwamba duka lake-

(a) ni jengo la kudumu lenye ukubwa usiopungua futi 10 kwa futi 12 na sakafu ya marumaru nyeupe;

(b) kuta zote za ndani ziwe na marumaru nyeupe;

(c) lina bomba la maji moto na maji baridi safi, na misumeno ya umeme ya kukatia nyama;

(d) liwe na mlango wa vioo, jokofu la kuhifadhia nyama na sehemu za mizani;

(e) liwe na pipa la kuhifadhia taka;

(f) muuzaji avae koti safi jeupe aproni, kofia na viatu vyeupe;

(g) muuzaji apime afya yake kabla na kila baada ya miezi sita katika vituo vya afya vya Halmashauri na kupatiwa cheti;

Utengenezaji na uuzaji vyakula

25.- Mtu yeyote hataruhusiwa kutengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha na kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote mpaka awe ametimiza masharti na kanuni za afya.

Uuzaji vyakula vilivyopikwa

26.- Kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye

sanduku lililotengenezwa kwa aluminium au mbao safi na kuwekwa kioo kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

Usalama wa matumizi ya maji

27.- (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji.

(2) Kila mmiliki wa kisima atapaswa kuhakikisha maji ya kisima yamepimwa ili yawe salama kwa matumizi;

Uzuiaji wa shughuli wakati wa magonjwa ya mlipuko

28.- Mkurugenzi anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

Ukamataji vyombo vilivyotumika kuhifadhia chakula wakati wa zuio

29.(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata vyakula, vyombo au vifaa vingine vyovyote vitakavyo kuwa vinatumika mara baada ya kutolewa amri ya zuio la kufanyika kwa shughuli ya uuzaji wa vyakula

wakati wa magonjwa ya mlipuko.

(2) Endapo vyakula vitakavyo kamatwa vitakuwa ni vile ambavyo vinaweza kuharibika kwa haraka Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuviharibu.

(3) Bila kuathiri masharti ya Aya Ndogo ya (1) na (2), endapo vyakula vilivyokamatwa vitakuwa haviharibiki kwa haraka Halmashauri itakuwa na jukumu la kuvihifadhi hadi mwisho wa amri ya zuio.

(4) Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Upimaji wa afya

30-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa biashara ya chakula, mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, bucha za samaki wabichi na wakavu, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari, maduka ya maziwa au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza kuhakikisha wahudumu wanapima Afya kila baada ya miezi sita.

(2) Mtu yeyote anayetengeneza ama kuandaa chakula kwa ajili ya kuuza ama kutoa huduma analazimika kupima afya yake kabla na baada ya miezi sita na atalipa ada ya Shilingi elfu tatu (3,000/=).

(3) Mmiliki yeyote atakayeruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya na kuvaa sare

kamili atakuwa ametenda kosa.

Uwezo wa kukagua

31.- (1) Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote wa saa za kazi na kwa ajili ya kufanya ukaguzi na kusimamia utekelezaji wa sheria Ndogo hizi.

(2) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Uendeshaji wa biashara ya nyumba za kulala wageni na hosteli

32.- (1) Itakuwa ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba za kulala wageni na hosteli kuhakisha jengo lake linafanyiwa ukaguzi wa kiafya na kupata idhini ya kuanza biashara baada ya kukidhi kanuni za afya.

(2) Endapo mmiliki hajakidhi masharti ya kiafya Halmashauri inaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya nyumba za kulala wageni au hosteli mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti yaliyotolewa na Halmashauri.

Mahitaji ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, hoteli na hosteli

33. Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, Hoteli na Hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa katika majengo hayo kuna:

(a) hewa ya kutosha;

(b) nafasi na vifaa (samani) za kutosha;

(c) uimara wa jengo;

(d) mfumo wa uondoshaji maji taka na taka ngumu wa kuaminika;

(e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;

(f) vyoo na mabafu kwa jinsia zote;

(g) vifaa vya zima moto;

(h) tanki la kuhifadhia maji safi; na

(i) vyoo na bafu vilivyosakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita kutoka usawa wa sakafu;

Kufungwa kwa jengo la biashara lisilokidhi masharti ya afya

34.- Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.

Ada ya ukaguzi wa kiafya katika jengo

35.- Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara ambayo viwango vyake vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kulipa ada

36.- Ada ya ukaguzi wa kiafya wa jengo italipwa kila mwanzo wa maombi mapya ya biashara yoyote na wakati wa marudio ya leseni.

Uanzishwaji wa vikundi jamii

37.-(1) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa vikundi vya jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), majukumu ya vikundi vya jamii yatakuwa ni

(a) kukusanya, kuzoa na kusafirisha taka kutoka maeneo yote ya uzalishaji na kuzipeleka katika eneo lililotengwa kwa ajili ya utupaji taka;

(b) kukusanya ada ya usafirishaji na uondoshaji taka katika maeneo ya makazi na biashara na kuwasilisha kiasi kilichokusanywa kwenye mfuko wa mazingira wa kata husika ambapo 70% ya mapato ya ada itatumika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za usafi za kikundi husika na 20% itabaki kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa shughuli za dampo la kisasa na 10% itabaki kwa ajili ya shughuli za ofisi ya kata na vitongoji husika.

Uhifadhi maji taka

38.- Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

39.- (1) Kila mmiliki wa nyumba au mpangaji atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba-

(a) nyumba yake ina choo bora na safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote;

(b) anaweka sehemu maalum ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni maalum ya kimiminika.

(2) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa zaidi ya mita sitini (60) kutoka katika kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani.

Vyoo vya umma

40.- (1) Halmashauri inaweza kujenga choo cha umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.

(2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na mawakala watakopewa kusimamia vyoo hivyo.

(3) Vyoo vitakavyojengwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitatakiwa kiwe cha kudumu na:

(a) matundu yasiyopungua mawili (2) kwa wanawake na mawili (2) kwa wanaume;

(b) mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji

ya kutosha yaliyo safi na salama;

(c) kuwepo na chombo cha kuhifadhia maji ya akiba;

(d) kuwepo kwa bafu ya wanaume na wanawake;

(e) kuwepo na chumba maalum cha kuvutia sigara;

(f) kuwepo na sehemu ya haja ndogo kwa wanaume; na

(g) kuwepo na chombo maalum chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

41.- Itakuwa ni wajibu wa kila mtu, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano au sherehe au mkusanyiko wowote kuweka au kujenga vyoo vya muda kwa matumizi ya wakati huo endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu na atatakiwa kuomba idhini na usimamizi kutoka Halmashauri.

Vyoo katika majengo ya biashara

42.- Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hii kwa ajili ya matumizi ya wateja wake kwa kuzingatia jinsi zote na wenye uhitaji maalum.

Ilani ya kujenga au kurekebisha choo

43.- Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo

kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, afisa mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba au mpangaji akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Ilani ya kuondoa kero

44.- (1) Endapo afisa mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ndani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Halmashauri kuteua mkaguzi

45.- Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote kuwa mkaguzi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa usafi wa mazingira katika eneo la Halmashauri.

Uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo

46.- Mkaguzi atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa mtu yeyote atakayekutwa amechafua mazingira, kwa kutupa taka mahali pasiporuhusiwa ilimradi adhabu hiyo izingatie masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Uteuzi wa Wakala

47.- (1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni kama

wakala wake wa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala atakayeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa kutekeleza yote yaliyomo kwenye mkataba wake wa uwakala.

Makosa

48.- Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii endapo:

(a)atamzuia au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia afisa mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) atatupa taka au uchafu wowote au kuacha taka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo;

(c) atamwaga taka barabarani, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, au mahali popote hadharani au katika eneo lolote lisiloruhusiwa;

(d) ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;

(e) atatiririsha maji machafu barabarani au katika

eneo la nyumba ya jirani;

(f) atafanya matengenezo ya magari au pikipiki au mitambo au kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(g) ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au nyumba ya makazi au maeneo yasiyoruhusiwa;

(h) ataosha magari au kufua au kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo cha maji au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;

(i)atapika au kuuza vyakula pembezoni mwa barabara au nje ya majengo mengine;

(j) ataenda haja ndogo au kubwa hovyo barabarani, uchochoroni au upenuni au mahali popote ambapo siyo chooni;

(k) atashindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

(l) atachanganya vyakula vibichi na vilivyopikwa kwenye jokofu;

(m) atasafirisha nyama kwenye mifuko ya sandarusi;

(n) atafanya maziko ya marehemu kwenye eneo la makazi ama taasisi;

(o) atauza chakula chochote bila kuvaa sare kamili;

(p) kuhamia na kuishi kwenye nyumba isiyokuwa na choo;

(q) atauza vyakula maeneo yasiyo rasmi na kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;

(r) ataacha nyumba anayoishi au kumiliki au kufanyia shughuli zake katika hali ya uchafu yenye kuleta kero au chukizo;

(s) ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu;

(t) ataendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;

(u) atafanya biashara ya kuosha gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli

hiyo au kuruhusu eneo lake kutumika kwa shughuli za kuosha vyombo vya moto katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hizo bila kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri;

(v) Mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji;

(w) Mtu yeyote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yoyote kwa namna yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe hai wengine ambao ni rasilimali ya taifa.

Adhabu

49.- Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyosidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote kwa pamoja.

kufifilisha makosa

Sura ya 287

50.- Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa mujibu wa Sheria, iwapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria

Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

---

**JEDWALI LA KWANZA**

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 35)*

**ADA YA UKAGUZI WA AFYA KATIKA JENGO**

| NAMBA | AINA YA BIASHARA | KIASI CHA ADA KWA MWAKA (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Baa na maduka ya vinywaji | 15,000/= |
| 2. | Migahawa au mama lishe | 10,000/= |
| 3. | Nyumba za wageni na hoteli | 15,000/= |
| 4. | Kumbi za starehe au mikutano | 15,000/= |
| 5. | Hoteli | 100,000/= |
| 6. | Kiwanda | 100,000/= |
| 7. | Majengo mengine ya biashara | 10,000/= |

---

**JEDWALI LA PILI**

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15)*

**ADA YA UZOAJI TAKA KWA KAYA, BIASHARA NA TAASISI**

*Tangazo la Serikali Na. 413 (Linaendelea)*

| NAMBA | AINA YA ADA YA TAKA | ADA KWA MWEZI (SHILINGI) |
|---|---|---|
| 1. | Kaya | 1,000/= |
| 2. | Mgahawa | 5,000/= |
| 3. | Nyumba ya Kulala Wageni | 5,000/= |
| 4. | Zahanati (Taka zisizo hatarishi) | 10,000/= |
| 5. | Kituo cha Afya (Taka zisizo hatarishi) | 10,000/= |
| 6. | Hospitali (Taka zisizo hatarishi) | 20,000/= |
| 7. | Kiwanda cha mbao | 10,000/= |
| 8. | Fundi Seremala | 5,000/= |
| 9. | Huduma za Uchomeleaji | 10,000/= |
| 10. | Karakana nyinginezo | 10,000/= |
| 11. | Kiwanda kidogo | 10,000/= |
| 12. | Kiwanda kikubwa | 30,000/= |
| 13. | Duka la jumla | 10,000/= |
| 14. | Duka la rejareja au huduma | 5,000/= |
| 15. | Shule ya Msingi ya bweni | 20,000/= |
| 16. | Shule ya Sekondai ya bweni | 20,000/= |
| 17. | Kituo cha kulelea Watoto | 10,000/= |
| 18. | Duka dogo la chakula | 5,000/= |
| 19. | Duka kubwa la chakula | 10,000/= |
| 20. | Baa | 10,000/= |
| 21. | Klabu za usiku | 10,000/= |
| 22. | Kituo cha burudani au kumbi za starehe na sherehe | 10,000/= |
| 23. | Duka la nyama na Samaki | 10,000/= |
| 24. | Nyama choma au chipsi inayojitegemea | 5,000/= |
| 25. | Duka la dawa la jumla na rejareja | 10,000/= |
| 26. | Duka la dawa la rejareja | 5,000/= |
| 27. | Dobi mdogo (mikono) | 2,000/= |
| 28. | Dobi mkubwa (laundry) | 10,000/= |
| 29. | Fundi vifaa vya umeme | 2,000/= |
| 30. | Fundi kushona kwa kila cherehani | 500/= |
| 31. | Kutengeneza nywele (Saluni) | 3,000/= |
| 32. | Kituo cha kuuza mafuta na vilainishi vya magari na mitambo | 20,000/= |
| 33. | Stoo mbalimbali | 5,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 413 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 34. | Ghala | 10,000/= |
| 35. | Hoteli | 20,000/= |
| 36. | Taasisi kubwa za kifedha (Benki, Saccos na Taasisi za Mikopo) | 20,000/= |
| 37. | Taasisi ndogo za kifedha (Wakala) | 20,000/= |
| 38. | Kilabu ya pombe za kienyeji | 3,000/= |
| 39. | Kituo cha kulaza wageni (hosteli) | 10,000/= |
| 40. | Kituo cha mazoezi ya viungo (Gym) | 5,000/= |
| 41. | Kiwanja cha michezo | 10,000/= |
| 42. | Fundi viatu | 2,000/= |
| 43. | Stoo ya mkaa | 10,000/= |
| 44. | Mama au Baba lishe | 3,000/= |
| 45. | Duka la kuuza magari | 30,000/= |
| 46. | Duka la madawa ya mifugo na sana za kilimo na pembejeo za jumla | 5,000/= |
| 47. | Duka la madawa kya mifugo na zana za kilimo na pembejeo za rejereja | 3,000/= |
| 48. | Studio ya picha | 3,000/= |
| 49. | Maeneo ya kuuza mbao | 5,000/= |
| 50. | Duka la mitambo na mashine | 5,000/= |
| 51. | Mashine ya kukoboa na kusaga nafaka | 5,000/= |
| 52. | Mashine ya kukamua mafuta | 5,000/= |
| 53. | Kiwanda cha mikate | 5,000/= |
| 54. | Duka la shajala | 5,000/= |
| 55. | Duka la vifaa vya ujenzi | 10,000/= |
| 56. | Ofisi ya kampuni au ushauri | 10,000/= |

---

**JEDWALI LA TATU**

---

*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 15(2)*

**GHARAMA ZA UTUPAJI WA TAKA KATIKA JALALA LA HALMASHAURI**

| NAMBA | AINA YA TAKA | KIASI CHA TAKA | KIWANGO CHA ADA (SHILINGI) |
|---|---|---|---|
| 1. | Taka za nyumbani | Zaidi ya tani moja<br>Chini ya tani moja | 50,000/=<br>40,000/= |
| 2. | Taka za viwandani | Zaidi ya tani moja<br>Chini ya tani moja | 70,000/=<br>50,000/= |
| 3. | Taka hatarishi | Zaidi ya tani moja<br>Chini ya tani moja | 100,000/=<br>80,000/= |

---

**JEDWALI LA NNE**

---

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 50)*

**FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA**

Mimi ……………………………………………………… nakiri **KWA HIARI YANGU MWENYEWE** mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ………… ya Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

**MBELE YANGU**:

Jina: …………………………………..……………………

Saini………………………..………………………..………

Wadhifa: …………………………………………………………

Tarehe…………………………………………………..………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Same imeandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 05 Mwezi Mei Mwaka 2023 Mbele ya;

ANASTAZIA TUTUBA
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Same*

YUSTO M. MAPANDE (DIWANI)
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Same*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma.
25 Machi, 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa nchi ofisi ya Rais*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*